

Wakazi wa Dar wanasemaji kuhusu afya?

Huduma za afya na utendaji katika Dar es Salaam



Utangulizi

Utafiti wa Kidemografia na Afya Tanzania (Tanzania Demographic and Health Survey (DHS)) wa mwaka 2010 unaonyesha uborekaji mkubwa katika mambo kadhaa ya msingi ya afya; kwa mfano, kiwango cha vifo vya watoto vimepungua na kuna kuongezeka kwa matumizi ya vyandarua ili kujikinga na malaria. Lakini viashiria vingine vinalegalega. Kwa mfano, pungufu ya watoto wanne katika 10 walio chini ya miaka 5 wanapata dawa sahihi ya kutibu malaria (*dawa ya mseto*; DHS, 2010), na Utafiti wa Viashiria vya Upatikanaji wa Huduma (SDI) ulionyesha kwamba kiasi cha robo tu ya dawa zote za msingi zilipatikana katika vituo vya afya ya serikali.

Je, kuna mambo gani yanatokea katika huduma za msingi za afya katika Dar es Salaam, jiji kubwa kuliko yote nchini Tanzania, na wakazi wa Dar es Salaam wanafikiri nini kuhusu huduma za afya wanazotumia?

Ili kujibu maswali haya na mengine, Uwazi iliyopo Twaweza ilifanya utafiti wa upatikanaji wa huduma kwa wananchi katika Agosti na Septemba 2010. Jumla ya kaya 550 zilizochaguliwa kinasibu walitembelewa na timu ya watafiti katika wilaya za Ilala, Temeke, na Kinondoni. Watafiti waliuliza maswali kuhusu namna wananchi wanavyoishi na uzoefu wao kuhusu huduma za jamii. Ili kuelewa uzoefu wa wananchi katika upatikanaji wa huduma za afya, wahojiwa waliulizwa



Muhtasari huu umeandikwa na Kevin Croke chini ya uangalizi wa Rose Aiko, na kuchapishwa na Uwazi iliyopo Twaweza –Hivos Tanzania.

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe: uwazi@twaweza.org.
Tovuti: www.twaweza.org/go/uwazi



kuhusu magonjwa yaliyotokea katika familia zao, uzoefu wao wa siku za hivi karibuni kuhusu huduma za afya, mtazamo wao na namna wanavyofanya mambo kuwiana na huduma za kuzuia magonjwa zinazotolewa. Muhtasari huu unawasilisha mambo muhimu kutoka katika ufafiti huu.

Mambo saba kuhusu afya Dar es Salaam


Ukweli wa 1: Karibu watu wote wana vyandarua vya kuzuia mbu

Ugonjwa wa malaria ni tatizo kubwa la afya na hatua ya msingi ya kinga inayoweza kuchukuliwa na kila kaya dhidi ya ugonjwa huo ni kulala ndani ya chandarua. Jambo hili ni muhimu zaidi kwa watoto wa umri chini ya miaka 5 na wanawake wajawazito. Suala la kusambaza na kuhimiza matumizi ya vyandarua limepewa kipaumbele na Wizara ya afya na Ustawi wa Jamii katika Tanzania. Utafiti huu umebaini kuwa katika kiwango cha kaya katika Dar es Salaam karibu watu wote wana vyandarua; asilimia 95 ya kaya wamesema kwa kiwango cha chini wanamiliki chandarua kimoja.

Ukweli wa 2: Ni nusu tu ya wakazi wa Dar es Salaam wanaochemsha au kutia dawa kwenye maji yao ya kunywa.

Baadhi ya magonjwa yanayotokana na maji ni kama vile kipindupindu na homa ya matumbo ambayo huwasumbua Watanzania yanaweza kuepukika kwa kutumia njia rahisi za kinga. Kwa kawaida ni wakazi wachache katika Dar es Salaam wanaoweza kupata maji safi. Kwa mfano, ni asilimia 9.7 tu ya kaya zote wanapata maji yao kupitia maboza yanayosambaza maji majumbani au wanaotumia maji ya kunywa ya chupa ya kununua. Lakini hata maji yanapoonekana ni safi pale yanapopatikana katika chanzo chake yanapofikishwa nyumbani yanaweza kuwa si salama. Hali hii inafanya kuweka dawa ya klorini kwenye maji au kuyachemsha kabla ya kunywa kuwa hatua muhimu ya kinga kwa wananchi walio wengi. Hata hivyo, ni nusu tu (asilimia 54) ya wale waliohojiwa ndio waliosema kuwa wanaweka dawa kwenye maji yao. Vile vile, hali hii inatofautiana sana kulingana na vipato vya wananchi: asilimia 75 ya wakazi katika kundi la wenye kipato cha juu wanaweka dawa kwenye maji yao au wanayachemsha ilikinganishwa na asilimia 23 ya wale walio katika kundi la wenye kipato cha chini kabisa.

Kielelezo cha 1: Asilimia ya kaya zinazochemsha au kuweka dawa kwenye maji ya kunywa




Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Ukweli wa 3: Kaya moja katika kaya tatu ilikuwa na mwanakaya mgonjwa katika juma moja kabla ya utafiti

Magonjwa ni hali ya kawaida katika kaya nyingi za Dar es Salaam. Asilimia 32 ya kaya zilizohojiwa walikuwa na mwanakaya angalau mmoja aliyeugua katika juma moja kabla ya utafiti. Kiasi cha theluthi moja ya muda huo mgonjwa huyo alikuwa ni mtoto mdogo sana. Karibu wanakaya wagonjwa 9 katika 10 (asilimia 86) walipelekwa katika kituo cha afya kupata matibabu.

Kielelezo cha 2: Kuwepo kwa mwanakaya mgonjwa, juma moja kabla ya utafiti

■ Kuna mwanakaya mgonjwa ■ Hakuna mwanakaya mgonjwa




Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Ukweli 4: Kaya masikini ndizo zenye uwezekano mkubwa wa kuhudumiwa katika vituo vya afya vya serikali

Katika Dar es Salaam kuna mahali pengi ambapo huduma za ushauri wa afya na matibabu hupatikana: maduka ya dawa, kliniki na hospitali za watu binafsi, zahanati za serikali na vituo vya afya, na hospitali. Wahojiwa wengi (asilimia 60) katika utafiti wamesema wanapokuwa na mwanakaya mgonjwa wao wanatumia vituo vya afya vya serikali. Asilimia 37 walisema wanapata huduma katika vituo vya afya vya watu binafsi, na asilimia 3 walisema wanakwenda kupata huduma katika vituo vya afya vinavyoendeshwa na mashirika ya dini au mashirika mengine yasiyo ya kiserikali.

Hali ya kiuchumi ya kaya ndiyo inayoamua mahali wanakaya watapokwenda kutibiwa. Kielelezo cha 3 kinaonyesha asilimia 82 ya kaya zenye kipato cha chini zinapata huduma kutoka vituo vya afya vya serikali ikilinganishwa na asilimia 27 ya kaya zenye kipato cha juu. Inaonekana kuwa jinsi kaya zinavyokuwa na kipato cha juu, ndivyo kaya hizo zisivyotumia huduma katika vituo vya afya vya serikali. Ni asilimia 16 tu kati ya kaya zilizo katika kundi la wenye kipato kidogo wanaopata huduma katika vituo vya afya vya watu binafsi ilikilinganishwa na asilimia 73 ya wakazi wenye kipato cha juu katika Dar es Salaam. Matokeo haya yanaonyesha kuwa ni wakazi walio na kipato cha chini wanaoumia wakati vituo vya afya vya serikali vinashindwa kutoa huduma bora kwa wagonjwa.

Kielelezo cha 3: Uchaguzi baina ya kituo cha afya cha serikali na cha watu binafsi kwa kundi la kipato




Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Ukweli 5: Vituo vya afya vya watu binafsi vinatoa huduma bora zaidi katika vipimo kadhaa vya ubora, na kutoa huduma inayowaridhisha zaidi wagonjwa

Ni vigumu kupima ubora wa huduma za afya kwa kutumia utafiti unaouliza wagonjwa au wanakaya hali ilivyokuwa wakati walipokwenda kutibiwa siku za nyuma. Hata hivyo, taarifa kuhusu ubora zinaweza kupatikana kwa kuuliza iwapo wagonjwa walifanyiwa vipimo walipomwona daktari, iwapo walishauriwa kuhusu jinsi matibabu ya matatizo yao ya afya yatakavyofanyika, na iwapo kwa maoni yao walihudumiwa kiheshima katika vituo vya afya. Kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo cha 4, kuna tofauti ndogo sana katika kila kipimo cha huduma kama ilivyotolewa kati ya hospitali za serikali na zile za watu binafsi kulingana na vipengele vya msingi vya mahudhurio yao katika kituo cha afya. Kwa upande mwingine, wagonjwa 8 katika 10 wanaridhika na huduma katika vituo vya afya vya watu binafsi, ikilinganishwa na wagonjwa 6 katika 10 wanaosema wameridhika na huduma katika vituo vya afya serikali.

Kielelezo cha 4: Taarifa kuhusu mashauriano ya kiafya katika kituo cha afya kulingana na aina ya kituo




Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Ukweli wa 6: Robo ya mahudhurio katika vituo vya afya vya serikali yaliyachukua muda wa kusubiri wa masaa mawili

Kwa nini wakazi wa Dar es Salaam wamesema wanapendelea kutibiwa katika vituo vya afya vya watu binafsi? Moja ya sababu inaweza kuwa ni kutokana na muda wa kusubiri: huduma hupatikana kwa haraka zaidi katika vituo vya afya vya watu binafsi ikilinganishwa na vituo vya serikali. Asilimia 80 ya wagonjwa walihudumiwa ndani ya dakika 30 katika vituo vya afya vya watu binafsi, ikilinganishwa na asilimia 31 katika vituo vya afya vya serikali. Robo ya wale waliohojiwa wamesema walisubiri kwa saa mbili au zaidi katika vituo vya afya vya serikali, na asilimia 16 walisubiri kwa zaidi ya saa tatu.

Kielelezo cha 5: Muda wa kusubiri katika kituo cha afya, kulingana na aina ya kituo




Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Ukweli wa 7: Mkazi mmoja katika watano alilazimika kutoa rushwa katika kituo cha afya cha serikali

Sababu nyingine kwa nini wakazi wa Dar es Salaam wanapendelea kutibiwa katika vituo vya afya vya watu binafsi (iwapo wanaweza kugharimia) inawezekana kuwa ni kutokana na kuenea kwa rushwa katika vituo vya afya vya serikali. Karibu mkazi mmoja katika wakazi watano katika Dar es Salaam amesema alitoa rushwa ili kupata huduma katika kituo cha afya cha serikali katika kipindi cha miezi 12. Ukweli kwamba ni lazima mgonjwa atoe rushwa ndipo apate huduma ina maana wakazi masikini hawawezi kupata huduma za kiafya wanazohitaji.

Kielelezo cha 6: Wahojiwa waliotoa rushwa katika kituo cha afya cha serikali katika mwaka uliopita

■ Alitoa rushwa ■ Hakutoa rushwa



Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Hitimisho

Muhtasari huu umewasilisha baadhi ya matokeo ya utafiti yanayohusu njia za kulinda afya na matumizi ya huduma za afya katika Dar es Salaam. Mambo tuliyogundua kwa upande mmoja yanaonyesha kwamba sera za serikali (yaani, usambazaji bure wa vyandarua) zimezisaidia kaya nyingi kulinda afya zao. Kwa upande mwingine, kuna idadi ya wakazi ambao bado hawachukui hatua za msingi za kujikinga na maradhi, kama vile kuchemsha maji ya kunywa au kuweka dawa. Vilevile wakazi wengi wanaona kwamba huduma za afya zinahitaji kuboreshwa: inaonekana kutoa rushwa ni jambo la kawaida sana katika vituo vya afya vya serikali na idadi kubwa ya wakazi hawaridhishwi na huduma wanazopata katika vituo hivi.

Hivyo mafanikio ya hivi karibuni kwenye sekta ya afya katika Tanzania huenda yamefikiwa kwa kuingilia kati kupitia mikakati ya kututua matatizo rahisi kwanza, kama vile kusambaza vyandarua vya kuzuia mbu. Kuongeza mafanikio zaidi

huenda kukawa kugumu kwa kuwa itahitaji kushughulikia vipengele mbalimbali vya ubora wa kutoa huduma, ikiwa ni pamoja na kubaini matatizo ya afya kwa usahihi zaidi, kuwaitikia wagonjwa, na kuboresha upatikanaji wa dawa. Hatua hizo vile vile ziambatane na kupunguza vikwazo vya kifedha (rushwa na ukwepaji wajibu) na uwajibikaji katika zahanati, vituo vya afya, na hospitali. Mahali bora pa kuanzia ni kuhakikisha kuna uwazi zaidi katika utoaji wa huduma za afya, rasilimali zilizopo na utendaji haki.